*Jarida La*

# MIFUGO NA UVUVI

*#mifugonauvuviniutajiri*

TOLEO NO; WMUV 0003| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

*Yaliyojiri Mwezi Machi 2025*

TSHS
**BIL. 460.3**
Ni bajeti iliyoidhinishiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2024/2025

- Ujenzi Jengo la Wizara umefikia asilimia 93
- Ujenzi Mwalo wa Chato Beach umefikia asilimia 91

# Kamati ya Bunge yapongeza Utekelezaji Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi 2024/2025



*Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu*

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni

HALIUZWI

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Yaliyomo *Ndani* Jarida


1 TAHARIRI .............**Uk. 04**

2 Kamati ya Bunge yaridhishwa utekelezaji Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi 2024/2025.......**Uk. 05 - 06**

3 Ujenzi Ghala la Malisho Mpwapwa Waikosha Kamati ya Bunge ........**UK 07**

4 Ujenzi Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi wafikia asilimia 93 ............. **Uk. 08**

5 Kamati ya Bunge yalitaja Jengo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa la mfano ........... **Uk. 09**

6 Matukio katika picha ya ziara ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwenye Miradi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi............ **Uk. 10**

7 Dkt. Kijaji awataka Watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa Wazalendo ...... **UK. 11**

8 Nchi 28 za Afrika zajadili mikakati kukabiliana dawa na chanjo feki za mifugo ........... **Uk. 12**

9 Majokofu 184 kugawiwa kwenye Halmashauri zote kwaajili ya zoezi la Chanjo............ **Uk. 13**

10 Mhe. Rais amechoka migogoro ya Wafugaji na wakulima - Mnyeti............. **Uk. 14**

11 Serikali yatangaza Mashamba ya Mifugo ni kwa ajili ya Wafugaji wa ndani tu........ **Uk. 15**

12 Ziwa Ikimba Kuvuna Tani 13 baada ya miezi 6 ....**Uk. 16**

13 Serikali yatambulisha mradi Mpya wa Tasnia ya Maziwa........**Uk. 17**

14 Dkt. Kimirei ateuliwa tena kuiongoza TAFIRI .. **Uk.18**

15 Prof. Shemdoe azindua mtambo wa kuzalishia barafu TAFICO........... **Uk. 18**

16 Rai yatolewa kwa Wafugaji wa Samaki kwenye Vizimba kushikwa mkono zaidi........... **Uk. 19**

17 Dkt. Kijaji aitaka Bodi ya TVLA kusimamia nidhamu za Watumishi........... **Uk. 20**

17 Kiwanda cha Samaki LIFA chatakiwa kuanza uzalishaji........... **Uk. 21**

18 Wanafunzi FETA wahimizwa kuchangamkia fursa ya mkopo ........... **Uk.22**

19 Wanafunzi wa SUA kujifunza kwa vitendo TAFIRI Kituo cha Dar es Salaam ........... **Uk.23**

20 Washiriki Mafunzo ya Ufugaji Samaki kwenye Vizimba waagizwa kuongeza uzalishaji...... **Uk.23**

21 Matukio katika Picha ya Shughuli mbalimbali zilizotekelezwa mwezi Machi na Viongozi, Wataalam na Wadau wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi...... **Uk.24 - 27**













# TAHARIRI

Machi 27, 2025 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuridhia mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Akizungumza kwenye kikao hicho bungeni jijini Dodoma, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Dkt. Medard Kalemani alipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo licha ya kuwa na bajeti ndogo lakini imeweza kutekeleza miradi ya kimkakati.

Aidha kamati hiyo iliiagiza wizara kuweka mazingira yatakayowafanya wananchi wanaojihusisha na mnyonyoro wa thamani katika sekta za mifugo na uvuvi waweze kunufaika na kuthaminiwa ili kuonesha umuhimu wa sekta hizo.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema kuwa wizara hiyo imeendelea kufanya vizuri na kuanza kuonekana ya thamani kwa jamii kutokana na usimamizi na ushauri mzuri unaotolewa na kamati hivyo wizara itaendelea kutekeleza miradi ya kuinua kipato cha mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa semina kuhusu upumzishwaji wa shughuli kwa Ziwa Tanganyika kwa Mwaka 2025 iliyofanyika katika ukumbi uliopo bungeni jijini Dodoma Machi 28, 2025 Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika alisema wizara iendelee kufanya utafiti katika ukanda wote wa Ziwa Tanganyika ili kubaini changamoto na kuzitatua.

Aidha Mhe. Mwanyika alipongeza serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuendelea kulinda rasilimali za taifa kwa manufaa ya wananchi wake na kusisitiza kuwa udhibiti wa uvuvi haramu ushughulikiwe kwa nguvu zaidi na kamati kuridhia upumzishwaji wa shughuli za uvuvi kwa Ziwa Tanganyika uendelee kulingana na manufaa yanayopatikana kutokana na takwimu zinavyoeleza.

Machi 18, 2025 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilipongeza pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa usimamizi mzuri wa fedha takriban Shilingi Milioni 219.7 zilizotumika kwenye ujenzi wa ghala la kuhifadhia malisho ya mifugo katika Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika mara baada ya kuiongoza kamati yake kukagua ghala hilo ambalo kukamilika kwake kutaifanya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kuhifadhi zaidi ya marobota 30,000 kwa wakati mmoja tofauti na awali ambapo maghala yake yaliweza kuhifadhi marobota 14,000 pekee.

Machi 14, 2025 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilipongeza viwango vya ubora wa ujenzi wa Mwalo wa Chato "Chato Beach" uliopo Wilaya ya Chato mkoani Geita ambao umefikia asilimia 91 hadi kukamilika kwake.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika mara baada ya kuongoza wajumbe kutembelea na kukagua ujenzi wa mwalo huo alitoa rai kwa taasisi nyingine za serikali kutafuta makandarasi wenye sifa za aina hiyo.

Machi 20, 2025 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifika katika ofisi za makao makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma na kupongeza hatua ya ujenzi wa ofisi za wizara.

Pongezi hizo zilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Mariam Ditopile muda mfupi baada ya kuiongoza kamati kukagua jengo hilo litakalogharimu takriban Shilingi Bilioni 24.9 hadi kukamilika kwake.

Hakika Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya uongozi wa Mhe. Waziri Dkt. Ashatu Kijaji imedhihirisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo namna inavyohakikisha inasimamia maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha sekta za uzalishaji zikiwemo za mifugo na uvuvi zinakuwa na tija kwa taifa na mwananchi mmoja mmoja


## Bodi ya Wahariri:

**Mwenyekiti**
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mhariri**
**Edward Kondela** - Afisa Habari Mwandamizi

**Msanifu**
**Hamis Hussein** - Afisa Habari

**Wajumbe**
**Elibariki Mafole** - Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike** - Afisa Habari
**Stanlay Bryaton** - Afisa Habari
**Chiku Makwai**- Afisa Habari




# Kamati ya Bunge yaridhishwa Utekelezaji Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi 2024/2025

## Yaahidi Kuisemea Wizaya hiyo kuongezewa Fedha

**Na, Hamisi Hussein, Omary Mtamike | WMUV, Dodoma**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, imepokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kuridhia mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Akizungumza Machi 27, 2025 kwenye kikao hicho Kaimu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Dkt. Medard Kalemani ameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo licha ya kuwa na bajeti ndogo lakini imeweza kutekeleza miradi ya kimkakati.

"Wizara hii huwa haipati bajeti kubwa sana ukilinganisha na wizara zingine lakini imeweza kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo inaenda kuleta tija kwa wananchi, hivyo Mhe. Waziri na watumishi wote wa wizara, sisi kamati tutaendelea kuishauri serikali ili iongeze bajeti kwenye sekta hii ya mifugo na uvuvi kwani inatoa utajiri kwa wananchi." alisema Mhe. Dkt. Kalemani.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema kuwa wizara hiyo imeendelea kufanya vizuri na kuanza kuonekana ya thamani kwa jamii kutokana na usimamizi na ushauri mzuri unaotolewa na kamati hivyo wizara itaendelea kutekeleza miradi ya kuinua kipato cha mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Mhe. Mwenyekiti wizara yetu inafanya vizuri kwa sasa na inaonekana kukua hii ni kutokana na ushauri na maelekezo ya kamati yako, hivyo tutaendelea kufanya kazi kwa weledi kuzikuza sekta hizi, hilo ndilo lengo letu." alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

### Upumzishwaji wa Shughuli za Uvuvi Ziwa Tanganyika

Katika hatua nyingine Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeridhia upumzishwaji wa shughuli za uvuvi kwa Ziwa Tanganyika uendelee kulingana na manufaa yanayopatikana kutokana na takwimu zinavyoeleza.

Hatua hiyo ilijiri kufuatia semina ya wabunge wanaotoka mikoa inayozungukwa na Ziwa Tanganyika kuhusu upumzishwaji wa shughuli kwa Ziwa Tanganyika kwa Mwaka 2025 iliyofanyika bungeni Jijini Dodoma Machi 28, 2025 ambapo Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika alisema Wizara iendelee kufanya utafiti katika ukanda wote wa Ziwa Tanganyika ili kubaini changamoto na kuzitatua.

> *"Tunaomba tusisitize tatizo la Uvuvi Haramu (gilnet) lishughulikiwe kwa nguvu kubwa kwa kushirikisha taasisi zote*
>
> **Mhe. Deodatus Mwanyika**
> Mwenyekiti Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo



Aidha Mhe. Mwanyika aliipongeza serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuendelea kulinda rasilimali za taifa kwa manufaa ya wananchi wake na kusisitiza kuwa udhibiti wa uvuvi haramu ushughulikiwe kwa nguvu zaidi.

"Tunawapongeza nyie kwa kufanya zoezi hili la kupumzisha ziwa, kwa sababu tumeanza kuona manufaa, bado kuna changamoto lakini tunaelekeza mpango wa kupumzisha ziwa kadri mlivyojipangia uendelee na tunasisitize tatizo la uvuvi haramu lishughulikiwe kwa kushirikisha taasisi zote" alisema Mhe. Mwanyika.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema kuwa serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu manufaa yanayopatikana baada ya zoezi la upumzishwaji wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa wavuvi pamoja na jamii kwa ujumla ili kuondoa taharuki wakati wa zoezi hilo.

Sambamba na hayo upumzishwaji wa Ziwa Tanganyika ulifanyika Mei 15, 2024 hadi Agosti 15, 2024 ambapo kwa mwaka huu unatarajiwa kufanyia Mei 15, 2025 hadi Agosti 15, 2025.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo wakifuatilia semina iliyokuwa ikitolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu mpango wa serikali wa kupumzisha Ziwa Tanganyika. Semina hiyo ilifanyika Machi 28, 2025 bungeni jijini Dodoma.

## Ujenzi wa Mwalo wa Chato Beach ni wa Viwango, Kamati ikipongeza

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imepongeza viwango vya ubora wa ujenzi wa Mwalo wa Chato "Chato Beach" uliopo Wilaya ya Chato mkoani Geita ambao umefikia asilimia 91 hadi kukamilika kwake.

Pongezi hizo zilitolewa Machi 14, 2025 na mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika mara baada ya kuiongoza kutembelea na kukagua ujenzi wa mwalo huo ambapo alitoa rai kwa taasisi nyingine za serikali kutafuta makandarasi wenye sifa za aina hiyo.

"Mara nyingi huwa tuna mjadala mrefu sana tunapotembelea miradi ya aina hii lakini leo tumekaukiwa maneno kwa sababu tumekutana na mradi tuliothibitisha kweli umekamilika kwa asilimia 91." aliongeza Mhe. Mwanyika.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti alimweleza katibu mkuu wa wizara hiyo na watendaji wake kuhakikisha wanampa miradi mingine ya wizara mkandarasi huyo kutokana na kazi aliyoifanya kwenye ujenzi wa mwalo huo.

# Ujenzi Ghala la Malisho Mpwapwa Waikosha Kamati ya Bunge



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Mhe. Deodatus Mwanyika akieleza namna kamati yake ilivyoridhishwa na usimamizi wa mradi wa ghala la malisho ya mifugo lililopo Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma Machi 18, 2025. Kulia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji.

**Na, Omary Mtamike - WMUV, Mpwapwa**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa usimamizi mzuri wa fedha takriban Shilingi Milioni 219.7 zilizotumika kwenye ujenzi wa ghala la kuhifadhia malisho ya mifugo katika Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Deodatus Mwanyika mara baada ya kuiongoza kamati yake kukagua ghala hilo ambalo kukamilika kwake kutaifanya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kuhifadhi zaidi ya marobota 30,000 kwa wakati mmoja tofauti na awali ambapo maghala yake yaliweza kuhifadhi marobota 14,000 pekee.

"Sisi tunawapongeza sana wizara kupitia taasisi ya TALIRI kwa kazi mliyofanya, mmefanya vizuri lakini tukupongeze Mhe. Waziri kwa sababu mkandarasi wa hapa pia amefanya kazi nzuri hivyo tunaweza kusema usimamizi wa wizara hii kwenye miradi upo vizuri." alisema Mhe. Mwanyika.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji mbali na kuishukuru kamati hiyo kwa kuidhinisha bajeti iliyowezesha ujenzi wa ghala hilo, ameliahidi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kusimamia fedha zote zinazoidhinishwa wizarani hapo ili kuongeza tija kwa wafugaji na wavuvi.

Aidha Dkt. Kijaji alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuonesha kwa vitendo dhamira yake ya kufanya mapinduzi kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo mifugo pamoja na kuwezesha kupatikana kwa mbegu bora za mifugo na malisho ya mifugo hiyo.

Akielezea lengo la ujenzi wa ghala hilo Mkurugenzi wa Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo Dkt. Asimwe Rwiguza alisema mradi huo utasaidia upatikanaji wa malisho kwenye kituo hicho kwa kipindi chote cha mwaka, kulinda ubora na kupunguza upotevu wa malisho hayo kutokana na kukosekana sehemu sahihi ya kuyahifadhi.

> "Sisi tunawapongeza sana wizara kupitia taasisi ya TALIRI kwa kazi mliyofanya, mmefanya vizuri lakini tukupongeze Mhe. Waziri kwa sababu mkandarasi wa hapa pia amefanya kazi nzuri hivyo tunaweza kusema usimamizi wa wizara hii kwenye miradi upo vizuri."
>
> **Mhe. Deodatus Mwanyika**
> Mwenyekiti Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo

# Ujenzi Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi wafikia asilimia 93

## Serikali ikimlipa Mkandarasi Tsh.Bilioni 18.15 sawa na asilimia 78 ya gharama za mradi

Na, Hamisi Hussein - WMUV, Dodoma

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte amemhimiza mkandarasi kusimamia ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kukamilisha sehemu zilizosalia.

Bw. Mhinte alisema hayo Machi 5, 2025 wakati akikagua ujenzi huo ambapo aliridhishwa hatua iliyofikiwa huku akiagiza kumalizika maeneo yaliyosalia kwa ubora pamoja na kutunza miundombinu ya jengo hilo.

"Wakati mnaendelea na shughuli zenu ni muhimu mkawa mnatunza miundombinu ya jengo hili ili kuepuka ukarabati kabla hata ya kuhamia." alisema Bw. Mhinte.

Pamoja na maelekezo hayo Bw. Mhinte aliridhishwa na hatua ya ujenzi huo ulipofikia jambo ambalo litarahisisha huduma kwa wananchi kama ilivyopangwa na serikali.

Kwa upande wake mbunifu majengo Kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Bw. Jona Mkogo alisema jengo hilo ambalo linagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 23.2 limefikia asilimia 93 hadi sasa na serikali imelipa kiasi cha Shilingi Bilioni 18.15 sawa na asilimia 78 ya gharama za mradi huo.

Ujenzi huo wa Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, unasimamiwa na Shirika la Taifa la Nyumba NHC huku wakala wa Majengo Tanzania (TBA) akiwa mshauri elekezi.



Muonekano wa Jengo la Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi lililopo katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma linalojengwa na Shirika la Taifa la Nyumba NHC ambalo Ujenzi wake umefikia asilimia 93 baada ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte kukagua Jengo hilo Machi 05, 2025.







# Kamati ya Bunge yalitaja Jengo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa la Mfano

## Rai ikitolewa kwa Serikali na Wadau kuamini Wakandarasi wazawa Ujenzi wa Miradi

**Na, Omary Mtamike - WMUV, Dodoma**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imepongeza hatua ya ujenzi wa Ofisi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi inayoendelea kwenye Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Pongezi hizo zilitolewa Machi 20, 2025 na Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Mariam Ditopile muda mfupi baada ya kuiongoza kamati kukagua jengo hilo litakalogharimu takriban Shilingi Bilioni 24.9 hadi kukamilika kwake.

"Kwa niaba ya kamati nzima kwa kweli niipongeze sana wizara kwa sababu tumejionea jengo hili limekidhi vigezo vyote vya kitaalamu lakini wamejiongeza limekuwa la kisasa mno na tumeoneshwa miundombinu ya gesi na maji kwa ajili ya kuzima moto na wamekidhi pia vigezo kwa kuweka miundombinu kwa watu wenye mahitaji maalum." alisema Mhe. Ditopile.

Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji mbali na kuishukuru kamati kwa ushirikiano waliyoipa wizara wakati wote wa ziara alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zilizotumika kujengea ofisi hiyo ambapo aliahidi wizara yake kuendelea kutoa huduma bora zaidi mara watakapohamishia shughuli zote kwenye jengo hilo.

"Sisi kama wizara tumejisikia faraja sana kwa sababu wabunge ni wawakilishi wa wananchi hivyo tunaona jicho la wananchi limeridhika na kazi yetu." aliongeza Mhe. Dkt. Kijaji.

Naye mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo Mhe. Ezra Chiwelewa alitoa rai kwa taasisi nyingine kuwa na imani kwa makandarasi wazawa kama ilivyofanya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambalo linatekeleza mradi huo kwa viwango bora.

Akizungumzia hatua za ujenzi zilizosalia kwenye jengo hilo, Mbunifu Majengo kutoka Wakala ya Majengo Tanzania (TBA) ambaye pia ni Mshauri Mwelekezi wa mradi huo Bw. Jona Mgogo amesema kuwa mpaka sasa wamefikia asilimia 93 ya ujenzi wa jengo hilo ambapo alibainisha kuwa kazi kubwa iliyosalia ni umaliziaji wa utengenezaji wa tanki kubwa la kuhifadhia maji chini ya jengo na uwekaji wa vioo.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## Ziara ya Kamati ya Bunge, Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo,Kwenye Miradi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi













# Dkt. Kijaji awataka Watumishi Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa Wazalendo

## Ataka watumishi kuwatumikia vyema wananchi

**Na, Stanley Brayton –WMUV, Dodoma**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, amewataka watumishi wa wizara hiyo kuwa na utumishi wa kizalendo uliotukuka kwa watanzania ili kuweza kusonga mbele katika sekta hizo mbili.

Akizungumza na watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Machi 26, 2025 katika Kikao chake na watumishi hao, kilicho jumuisha wakuu wa idara, vitengo na taasisi za wizara, kilichofanyika katika ofisi za Makao Makuu ya Wizara katika Mji wa Kiserikali Mtumba, jijini Dodoma, Dkt. Kijaji alisema anafurahishwa na utendaji mzuri wa watumishi wa wizara hiyo huku akiwapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi.

"Wizara inaonekana jinsi inavyofanya kazi na inaendelea kufanya kazi vyema kwani tangu tuanze kuzunguka na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, tulikopita kwenye miradi yetu yote walitupongeza na kusema tumefanya vizuri" alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

Aidha, Dkt. Kijaji alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Vilevile, Dkt. Kijaji alisema matarajio na matumaini ni makubwa katika sekta za mifugo na uvuvi kwa sababu Mhe. Rais tangu aingie madarakani ameamua kuzipa kipaumbele sekta za uzalishaji zikiwemo sekta hizi mbili, ambazo ndiyo sekta zinazogusa maisha ya kawaida ya watanzania hususani walio katika maisha ya chini.

Dkt. Kijaji aliwaelekeza watendaji wa wizara kuhakikisha wanasimamia maeneo yote ya mifugo na malisho na kuainisha maeneo hayo pamoja na kuwaita wafugaji kuwaelewesha umuhimu wa kumiliki ardhi na malisho.

Halikadhalika, Dkt. Kijaji aliwataka watendaji wa wizara kuanza zoezi la kuwarasimisha wavuvi wote nchini na kuwatambua wapo wangapi na wanafanya nini, ikiwa ni pamoja na kujua kuwa kuna vyombo vingapi vya uvuvi nchini.

"Wakuzaji viumbe maji tuwe na tathimini ya maji yote na kuamua kufanya kazi ipasavyo ili ndani ya miaka mitano ijayo pato kubwa la nchi hii litokane na Uchumi Buluu na hilo linawezekana." alisema Mhe. Dkt. Kijaji.



# Nchi 28 za Afrika zajadili Mikakati Bora Mapambano ya Dawa, Chanjo Feki za Mifugo

*Wafugaji, Wadau wa uzalishaji wa Chanjo watakiwa kuzingatia Sheria na Taratibu.*

**Na, Chiku Makwai- WMUV, Dodoma**

Nchi 28 zimekutana katika mkutano wa kimataifa wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH) kwa ukanda wa Afrika, kujadili na kuweka mikakati ya kudhibiti dawa na chanjo feki kwa mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mkutano huo uliofanyika Machi 4, 2025 jijini Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte alisema Tanzania iko tayari kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya dawa na chanjo feki za mifugo.

Mkutano huo wa siku tatu, kuanzia Machi 4 hadi 6, ulijadili mikakati mbalimbali ambayo wataalamu walichambua na kutoa maoni kuhusu namna bora ya utekelezaji katika kila nchi kulingana na taratibu zao.

"Mkutano huu ni muhimu kwa Afrika, kwani kumekuwa na ongezeko la dawa na chanjo feki, jambo lililosababisha WOAH kuandaa mkakati maalum wa kusaidia nchi za Afrika na dunia kwa ujumla kupambana na tatizo hilo." Alifafanua Bw. Mhinte

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Benezeth Lutege, alibainisha kuwa serikali imetenga Shilingi Bilioni 28.1 kwa ajili ya kampeni ya kitaifa ya chanjo kwa mifugo, ambayo itazinduliwa hivi karibuni.

"Chanjo zitakazotumika mwaka huu ni zile zinazozalishwa ndani ya nchi na kukaguliwa na mamlaka za serikali, hatua ambayo itasaidia kuzuia uingizwaji wa chanjo na dawa feki zinazosababisha usugu wa magonjwa," alisema Dkt. Lutege.

Aidha Dkt. Lutega aliwataka wafugaji, waingizaji wa dawa na chanjo, pamoja na wazalishaji, kuzingatia kanuni na taratibu za uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa dawa hizo.

Naye mwakilishi kutoka WOAH Bi. Jane Royelo aliwahimiza wafugaji na wauzaji wa dawa za mifugo kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuhamasishwa matumizi sahihi ya dawa na kuepuka matumizi mabaya ya dawa zisizohitajika.

Miongoni mwa mikakati iliyopendekezwa ni kuanzisha mifumo madhubuti ya usajili na ufuatiliaji wa dawa zinazoingizwa na kutumika hatua ambayo itasaidia kuziondoa dawa na chanjo zisizo na viwango stahiki sokoni.

# MAJOKOFU 184 KUSAMBAZWA KWENYE HALMASHAURI ZOEZI LA UCHANJAJI MIFUGO KITAIFA

## Dkt. Kijaji akiitaja Mikakati kufanikisha zoezi la Chanjo Kitaifa

**Na, Daud Nyingo - TVLA, Dar es Salaam**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kukamilisha maandalizi ya kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo kitaifa ambapo miongoni mwa maandalizi hayo majokofu 184 yatagawiwa katika Halmashauri 184 nchini ikiwa ni muendelezo wa kukamilisha maandalizi ya zoezi la kutoa chanjo kitaifa ili uchanjaji huo ufanyike kwa ufanisi.

Hayo yalibainishwa Machi 21, 2025 na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alipokuwa akipokea majokofu 60 yanayolenga kuboresha mnyororo baridi nchi nzima kutoka Kampuni ya Hester Bioscience Africa Ltd kwenye ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es Salaam.

Mhe. Dkt. Kijaji alisema kuwa mikataba na wazalishaji wa chanjo ilishasainiwa na kampuni tatu za ndani zikiwemo Hester Bioscience Africa Ltd, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na NOVAB ambapo moja ya makubaliano ilikuwa watoe majokofu kwa ajili ya kuhifahdi chanjo hizo ili zisiharibike.

"Kampuni ya Hester Bioscience Africa Ltd tulikubaliana watupatie majokofu 100 na leo hii wamekabidhi majokofu 60, tunawasisitiza wakamilishe yote 100. Vilevile tulishapokea majokofu 40 kutoka kampuni zingine ambazo yamepelekwa Mkoani Mwanza. Tutaendelea na zoezi hili ili tukamilishe maandalizi yote na tuanze zoezi letu la chanjo kwa mifugo yetu kama kuku, ng'ombe, mbuzi na kondoo kama ambavyo Mhe. Rais alivyoridhia na akatupatia bajeti ya Shilingi Bil. 28 kwa miaka mitano mfululizo." alisema Dkt. Kijaji

Kwa upande wake Mwekezaji wa Kampuni ya Hester Bioscience Africa Ltd Bw. Lajiv Gandhi alisema kuwa ni heshima kubwa kwa kampuni yao kuwepo kwenye mpango wa taifa wa uchanjaji pamoja na kupewa mkataba na wizara wa kusambaza chanjo kwa wafugaji.

"Imekuwa ni siku muhimu sana kwetu kuwemo kwenye uzinduzi wa mpango wa taifa wa chanjo wa Serikali ya Tanzania wa kuchanja wanyama hasa kwa chanjo ya PPR, CBPP, Ugonjwa Kideri, Ndui na Mafua kwa kuku. Tumejawa na heshima kubwa sana kwamba Wizara ya Mifugo imetupa mkataba na leo tunakabidhiwa majokofu 60 kwa ajili ya kuhifadhia" alisema Bw. Gandhi



Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Katikati) akikata utepe wakati akipokea Majokofu 60 ya Kuhifadhia Chanjo za Mifugo kutoka kwa Mwekezaji wa Kampuni ya Hester Bioscience Africa Ltd Bw. Lajiv Gandhi (wa tatu kulia) hafla iliyofanyika Ofisi ndogo za Wizara zilizopo Jijini Dar es Salaam Machi 21, 2025, Wengine ni Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte(Wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Dkt. Benezeth Lutege (Wa kwanza Kushoto).

*Mashamba ya kufugia Mifugo sio ya kilimo ni kwa ajili ya Wafugaji.*

# MHE. RAIS AMECHOKA MIGOGORO YA WAFUGAJI NA WAKULIMA: MNYETI



**Na. Hamisi Hussein – WMUV, Rukwa**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti amesema serikali imetoa mashamba ya kuzalishia mifugo ili kuwasaidia wafugaji kupata maeneo ya malisho yatakayoongeza tija kwa uzalishaji wa mifugo bora na kuondoa migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Akizungumza mara baada ya kukagua mashamba ya kuzalishia mifugo Ranchi ya Kalambo iliyopo Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa Machi 8, 2025, Mhe. Mnyeti alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amechoka kusikia migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima hivyo serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi itawanyang'anya watu wote waliopewa mashamba ya kuzalishia mifugo na badala yake kuyatumia kwa shughuli za kilimo.

"Kwa ukubwa wa eneo hili ekari 150,000 tunauwezo wa kuleta ng'ombe wa Mtwara, Lindi tukawapa wafugaji vitalu vya ekari mia tano mia tano kwa sababu tumechoka, Mhe. Rais amechoka migogoro ya wafugaji na wakulima." alisema Mhe. Mnyeti.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti akitoa msimamo wa serikali wa kuwaondoa wawekezaji waliopangishwa mashamba ya serikali ya kuzalishia mifugo Ranchi ya Kalambo waliokiuka mkataba kwa kuanza shughuli za kilimo cha mazao wakati wa ziara yake mkoani Rukwa Machi 8, 2025.

Aidha Mhe. Mnyeti aliiagiza Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuwaandikia notisi ya kuondoka kwenye mashamba ya kuzalishia mifugo wawekezaji walioshindwa kuyatumia mashamba hayo kwa ajili ya mifugo na badala yake wamekuwa wakiyatumia kwa shughuli za kilimo jambo ambalo ni kinyume na mkataba wa upangishaji.

Kwa upande wake Mwanasheria wa NARCO Bw. Saidi Seni alisema katika mkataba wa kuwapangisha wawekezaji hauruhusu shughuli za kilimo cha mazao tofauti na uzalishaji wa mifugo na malisho huku Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) Bw. Mrida Mshota akieleza hali ya uhitaji wa wafugaji wa mashamba hayo.

Ranchi ya Kalambo ina ukubwa wa hekta 64,650 zenye uwezo wa kuweka idadi ya ng'ombe zaidi ya 30,000 ambapo hadi kufikia mwezi Februari 2025 jumla ya hekta 29,465.96 zilikodishwa kwa wawekezaji wa mikataba ya muda mrefu ambayo ni miaka 33.

# Serikali yatangaza Mashamba ya Mifugo ni kwa ajili ya wafugaji wa ndani

**Na. Hamisi Hussein –WMUV, Kagera**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti ameiagiza Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) Kufanya tathmini ya mashamba ya serikali ya mifugo yaliyokodishwa kwa wawekezaji na wakiwabaini waliokodisha mashamba hayo kwa wafugaji kutoka nje ya nchi wavunje mikataba na kufuta umilikishaji wa mashamba hayo.

Mhe. Mnyeti alitoa agizo hilo Machi 10, 2025 katika ziara ya kikazi mkoani Kagera ambapo alisema serikali haitakuwa tayari kuruhusu wafugaji kutoka nje ya nchi kuingiza mifugo kwenye mashamba hayo ya serikali.

“ Wale ambao wamechukua vitalu vya serikali na wakakaribisha wafugaji kutoka nje ya nchi, NARCO nendeni mkavunje mikataba yao, maeneo hayo wapeni wafugaji waliopo ndani ya nchi.” alisema Mhe. Mnyeti.

Aidha Mhe. Mnyeti aliongeza kuwa serikali itawanyang’anya wawekezaji ambao hawana mifugo kwenye vitalu vya serikali ili kuwapa wafugaji wadogo wadogo ambao wamekuwa wakikodishiwa na wawekezaji wasio na mifugo kwenye vitalu hivyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Karagwe Mhe. Julius Kalanga alisema ili kuweza kudhibiti uvamizi wa mashamba ya serikali, NARCO ifanye utambuzi na usajili wa mifugo inayopatikana kwenye vitalu hivyo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa NARCO Dkt. Bwire Kafumu alisema mchakato wa utambuzi na usajili wa mifugo kwenye vitalu vya mashamba ya serikali ya mifugo umeshaanza ili kufikishwa katika mamlaka za serikali kwaajili ya zoezi la utambuzi kabla ya kutoa mikataba mipya ya upangishaji wa mashamba kwa wawekezaji.

Ziara ya kikazi ya Naibu Waziri Mhe. Mnyeti, kukagua hali ya mashamba ya serikali ya kuzalishia mifugo ilihitimishwa mkoani Kagera machi 10, 2025 huku ukaguzi wa mashambahayoukitarajiwa taendelea kwenye maeneo mengine lengo likiwa kuhakikisha mashamba hayo yanamnufaisha mfugaji.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe.Alexander Mnyeti (katikati) akitoa maelekezo kwa mwekezaji wa vitalu vya mifugo vya serikali ndani ya Ranchi za Taifa Karagwe Bw. Hamza Ibrahimu wakati wa ziara yake mkoani Kagera Machi 10, 2025.

> *Wale ambao wamechukua vitalu vya serikali na wakakaribisha wafugaji kutoka nje ya nchi, NARCO nendeni mkavunje mikataba yao, maeneo hayo wapeni wafugaji waliopo ndani ya nchi.*
>
> Mhe. Alexander **Mnyeti**
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi



# Ziwa Ikimba Kuvuna Tani 13 za Samaki baada ya Miezi 6

*Ni baada ya kupandikiza Vifaranga Milioni 1.5 vya Samaki aina ya sato*

**Na, Omary Mtamike - WMUV, Kagera**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amesema zoezi la upandaji vifaranga vya samaki Mil.1.5 kwenye Ziwa Ikimba lililopo mkoani Kagera litaongeza mavuno ya samaki aina ya sato kwa mwaka kwenye ziwa hilo kutoka tani moja inayovunwa hivi sasa hadi tani 13 baada ya miezi sita.

Mhe. Dkt. Kijaji alisema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa upandaji wa vifaranga hivyo na kukabidhi boti moja ya doria Machi 12, 2025 kwenye Mwalo wa Buterankuzi ambapo aliwataka wananchi wa kata zote zinazonufaika na ziwa hilo kulinda vifaranga hivyo ili waweze kunufaika na mavuno kwenye ziwa hilo.

“Lakini pia naelekeza wataalamu wangu kabla hamjaondoa, mfanye tathmini kama ndani ya Ziwa Ikimba kunaweza kufanyika ufugaji wa vizimba ili wananchi hawa wanufaike zaidi na uwepo wa ziwa hili.” alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

Aidha Mhe. Dkt. Kijaji alitumia fursa hiyo kutangaza upumzishwaji wa ziwa hilo kwa miezi sita ili kuvipa nafasi vifaranga hivyo kukua hadi kufikia hatua ya matumizi kibiashara huku pia akitangaza kufanyika kwa doria ya wakati wote kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali zilizopo kwenye ziwa hilo.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kaibanja ambayo ni miongoni mwa kata zinazohudumiwa na Ziwa Ikimba Mhe. Jackson Rwankomezi alisema hali ya upatikanaji wa samaki katika ziwa hilo kwa sasa haikidhi hata mahitaji ya chakula hivyo wananchi wameamua kwa hiyari zoezi hilo ili waweze kunufaika kijamii na kukuza uchumi wao.

> “ Naelekeza wataalamu wangu kabla hamjaondoa, mfanye tathmini kama ndani ya Ziwa Ikimba kunaweza kufanyika ufugaji wa vizimba ili wananchi hawa wanufaike zaidi na uwepo wa ziwa hili.
>
> **Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji**
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi




# Serikali yatambulisha Mradi Mpya Tasnia ya Maziwa

**Na. Stanley Brayton – WMUV, Dodoma**

Serikali imeendelea kufanya juhudi za kuimarisha na kuweka mikakati bora ya kukuza Tasnia ya Maziwa kwa kutambulisha mradi mpya wa kimageuzi wa tasnia hiyo.

Akizungumza katika warsha fupi ya kutambulisha mradi huo Machi 17, 2025 jijini Dodoma, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, alisema mradi huo utagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 174.36 na utakuwa muhimu sana kwa watanzania wengi.

"Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kuwepo kwa mradi huu ambao utasaidia kunyanyua uchumi wa watanzania na nchi kiujumla." alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, Prof. Shemdoe alielekeza kuwa mradi huo uzingatie thamani ya fedha, muda pamoja na matokeo chanya yanayolenga kuwanufaisha vijana, akinamama pamoja na makundi maalum. Vilevile, Prof. Shemdoe alieleza kuwa mradi huo ni muunganiko wa Tanzania Bara na Visiwani unaotarajiwa kufika katika mikoa 10 na wilaya 28.

Prof. Shemdoe aliwashukuru wadau wa maendeleo pamoja na wadhamini ambao ni IFAD, OPEC Fund, AFD, Irish League of Credit Union's Foundation (ILCUF), HEIFER, International Tanzania (HI), Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) na FAO.

> *Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kuwepo kwa mradi huu ambao utasaidia kunyanyua uchumi wa watanzania na nchi kiujumla.*
>
> **Prof. Riziki Shemdoe**
> Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Zanzibar, Bw. Ali Khamis Juma, alisema mradi huo unategemewa kuinua kipato na maisha ya mtanzania hususan kwa wafugaji kwani serikali imejipanga kushirikiana na wafugaji wadogo na kuwasaidia kukua katika Tasnia ya Maziwa.

Pia, Mkurugenzi wa Uzalishaji na Maendeleo ya Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bw. Stephen Michael, alisema maziwa yanahitaji kuchangia zaidi katika Pato la Taifa, japo kunahitajika kuhakikisha upatikanaji wa maziwa kwa wingi na inatakiwa kuwekwa kwa mazingira mazuri zaidi ikiwemo kuboresha malisho na upatikanaji wa maji, huduma za ugani, tafiti, mafunzo na masoko kwa ajili ya wafugaji.

Naye, Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Prof. George Msalya alisema Tasnia ya Maziwa ina changamoto nyingi zikiwemo za uzalishaji mdogo wa maziwa, masoko na ukusanyaji wa maziwa ambao unachangiwa sana na mabadiliko ya hali ya hewa,



# DKT. ISMAEL KIMIREI, ATEULIWA TENA KUIONGOZA TAFIRI

*Ni baada ya kumaliza Kipindi cha kwanza tangu ateuliwe 2020*

**Na.Herry Kilele - TAFIRI, Dar es Salaam**

Machi 12, 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alimteua tena Dkt. Ismael Kimirei kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI). Uteuzi huu unakuja baada ya Dkt. Kimirei kumaliza kipindi chake cha kwanza cha uongozi na kuonyesha mafanikio makubwa katika sekta ya uvuvi nchini.

Dkt. Kimirei aliteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAFIRI Mwaka 2020 ambapo katika kipindi chake cha kwanza, aliongoza juhudi za kuboresha utafiti wa uvuvi nchini Tanzania, ambapo alisisitiza umuhimu wa tafiti zinazofanywa na taasisi hiyo ili kuongeza tija na kuboresha mbinu za uvuvi.

Alifanya kazi kwa karibu na wavuvi, wataalamu wa uvuvi, na Serikali ili kuhakikisha kuwa tafiti zinazofanywa zinakuwa na mchango chanya katika kukuza kipato cha wavuvi, kuongeza uzalishaji wa samaki, na kuboresha uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na kukuza na kuendeleza uchumi mahili wa buluu.

# Prof. Shemdoe Azindua Mtambo wa Kuzalisha Barafu TAFICO

**Na Evaristh Mkahe - TAFICO, Dar es Salaam**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe amezindua mtambo wa kuzalisha barafu za tofali (block ice) wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), kwenye hafla ya makabidhiano na uzinduzi iliyofanyika Machi 07, 2025 katika Makao Makuu ya shirika hilo Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Prof. Shemdoe alisema mtambo huo wenye uwezo wa kuzalisha tani tano kwa siku uliokabidhiwa na Kampuni ya Albacore ya Afrika Kusini utasaidia kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kwa kuongeza upatikanaji wa barafu kwa matumizi ya shirika, wavuvi na wauzaji wa samaki kwenye Soko la Feri, Kilwa, Lindi na maeneo mengine.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu TAFICO CPA Shaibu Matessa alisema ujio wa mtambo huo ni muhimu kwani utawezesha kuendeleza utekelezaji wa miradi tisa iliyopo kwenye Mpango wa Biashara wa TAFICO wa miaka kumi (2023/2033), kati ya miradi hiyo ni uzalishaji wa barafu kwa ajili ya kusaidia kupunguza upotevu wa mazao ya Uvuvi baada ya kuvuliwa, hivyo kuongeza tija kwa shirika na wavuvi wengine.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) Dkt. Emmanuel Sweke, mwakilishi wa Kampuni ya Albacore, Bw. Andrew Thompson, wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali na wadau wengine wa uvuvi.



Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Riziki Shemdoe akizindua na kukagua mtambo wa kuzalisha barafu za tofali (block ice) wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), kwenye hafla fupi ya makabidhiano na uzinduzi iliyofanyika Machi 07, 2025 katika makao makuu ya shirika hilo jijini Dar es Salaam.



# Rai yatolewa kwa Wafugaji Samaki Kwenye Vizimba Kushikwa Mkono Zaidi

**Na. Edward Kondela – WMUV, Mara**

Serikali imetoa wito kwa wawekezaji na watoa huduma mbalimbali zikiwemo taasisi za kifedha kuungana na serikali pamoja na sekta binafsi ili kuwezesha wawekezaji wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba waendelee kufanya vizuri zaidi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede alibainisha hayo Machi 20, 2025 wakati alipofanya ziara ya kikazi katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara, kushuhudia maendeleo ya uwekezaji wa vizimba katika ukanda wa mkoa huo.

Akishuhudia uvunaji wa samaki aina ya sato wanaofungwa kwa njia ya vizimba kwenye Ziwa Victoria kupitia uwekezaji wa Kampuni ya GODWIN LUSASO General Supply ltd, Dkt. Mhede alitoa rai kwa wananchi kuwa na utaratibu wa kukusanya fedha kidogo kidogo na kuzihifadhi kwa kuwa mwekezaji huyo ametumia fedha zake mwenyewe na kwamba serikali itaendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili Sekta ya Uvuvi ikue zaidi.

Alifafanua kuwa mwekezaji huyo alianza na vizimba vitatu lakini hadi sasa ana vizimba 18 ambapo awamu hii ya kwanza anavuna kwenye vizimba sita na anachovuna kwa sasa kinalipa gharama za uwekezaji wote alioweka ikiashiria wazi namna biashara hiyo inavyolipa na kubainisha samaki hao ni bora.

“Tumekuja na wenzetu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) na Maabara ya Taifa ya Uvuvi (NFQCLAB) ambao kazi yao ni kufanya mapitio ya ubora wa samaki wanaovunwa hapa, ninawatoa wasiwasi watanzania hawa samaki hawana matatizo ya kimaabara ni bidhaa bora.” alisema Dkt. Mhede. Aliongeza kuwa wawekezaji wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba wataunganishwa katika masoko mbalimbali vikiwemo viwanda vya kuchakata samaki hivyo ni muhimu kuwepo na ushirikiano wa pamoja kati ya viwanda na wawekezaji ili kuwa na masoko ya uhakika.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mara, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma Bw. Juma Chikoka, alisema upande wa Musoma fursa ya uwekezaji kwa njia ya vizimba ipo kwa sababu eneo kubwa la Wilaya ya Musoma limezungukwa na utajiri wa Ziwa Victoria.

Bw. Chikoka alitoa wito kwa wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji na maeneo mengine nchini kuja kuwekeza ufugaji wa kisasa kwa njia ya vizimba kwa kuwa matokeo yake ni makubwa na hii inajenga fursa nyingine ya ajira na uchumi wa Manispaa ya Musoma na Musoma vijijini.

Aidha, alisema mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuwekeza katika ufugaji wa kisasa kwa njia ya vizimba hususan katika mkakati wa Uchumi wa Buluu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya GODWIN LUSASO General Supply ltd Bw. Godwin Kababaye alibainisha kuwa katika uwekezaji wake kwenye ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba awamu hii ya kwanza anavuna takriban tani 50 ambapo anachukua uwekezaji huo kama fursa kwake na ajira kwa wengine.

Bw. Kababaye aliongeza kuwa katika uwekezaji wake ametumia zaidi ya Shilingi Milioni 430 lakini anahitaji nguvu zaidi kwa kuwa matamanio yake ni kujenga kiwanda cha kuchakata samaki na kuiomba serikali kuweka nguvu zaidi katika upatikanaji wa chakula cha kutosha cha samaki na idadi kubwa ya vifaranga ya samaki na vyenye ubora ili wafugaji wa samaki waweze kufuga samaki wengi zaidi.

Katika ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede alipata pia fursa ya kutembelea vizimba vya mradi unaofadhiliwa na serikali kwa vikundi vidogo na kujionea maendeleo ya mradi huo.

# Dkt. Kijaji Aitaka Bodi TVLA Kusimamia Nidhamu kwa Watumishi

**Na. Daud Nyingo – TVLA, Dar es Salaam**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji ameitaka Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kuhakikisha inasimamia nidhamu watumishi wote ambao hawatekelezi majukumu waliyopangiwa.

Mhe. Dkt. Kijaji alibainisha hayo Machi 21, 2025 jijini Dar es Salaam, kwenye uzinduzi wa bodi hiyo ambapo aliisisitizia bodi kutosita kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi watakaothibitika kwenda kinyume na maelekezo ya serikali pamoja na watakaotengeneza mazingira ya kupata chochote kwenye huduma ambayo aliiomba kuwahudumia Watanzania.

"Tufanye kazi kwa uadilifu na uaminifu mkubwa, watanzania wanatutegemea sana. Sisi ni watoaji wa huduma lakini pia ni wadhibiti, baadhi ya taasisi zinajisahau kwenye utoaji huduma, zinajikita kwenye udhibiti. Kwa mwelekeo wa Serikali ya awamu ya sita, udhibiti ni lazima uwe wa kuwezesha uwekezaji na ufanyaji biashara, maelekezo tuliyonayo ni kuwezesha wawekezaji wetu." alisema Mhe. Dkt. Kijaji.

Mhe. Waziri aliitaka bodi hiyo itakapoandaa mpango mkakati mpya wa TVLA kujikita kwenye mpango wa Dira ya Taifa ya miaka 25 ijayo ili mpango wa wakala usomane na Dira ya Taifa inayoanza Mwaka 2026 - 2050. Sambamba na hilo Mhe.

Dkt. Ashatu Kijaji aliitaka bodi ya TVLA kuhakikisha inasimamia kwa ufanisi afya za mifugo nchini ambapo aliitaka wakala kuwa kituo cha umahiri kutoa bidhaa na kufanya tafiti za magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa ndani na nje ya nchi.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Bw. Abdul Mhinte alisema kuwa wizara ina taasisi nyingi kwenye Sekta ya Mifugo lakini TVLA ni taasisi mama kwani inachangia kwa kiasi kikubwa Sekta ya Mifugo isiyumbe kwa hiyo wizara kwa sasa inategemea uwepo wa bodi uwe na mchango mkubwa kwa maendeleo ya Sekta ya Mifugo.

"Kipindi hiki ambacho mmeteuliwa kwenye hii bodi kwa hakika tunategemea muiendeshe hii taasisi kiuchumi, na katika kuonesha hilo tumeona mnashiriki hata kwenye zabuni za kusambaza chanjo nchini. Tunategemea huko mbele tuendako, taasisi hii itafanya zaidi ya vile inavyofanyika na kwa uongozi wenu tunategemea taasisi hii mbali na kushiriki kwenye zabuni hapa nchini iwe na uwezo wa kushiriki hata nje ya Tanzania, tuweze kuuza chanjo nje na kutoa huduma. Kipindi hiki ni kipindi muhimu, na tunategemea mabadiliko makubwa kwenye taasisi yetu." alisema Bw. Mhinte.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri TVLA, Prof. Amandus Muhairwa alimshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji kwa kuwaamini na kuwateua kushika dhamana ya kusimamia na kushauri maendeleo ya TVLA ambayo ni taasisi muhimu katika uimarishaji wa afya za mifugo nchini.

"TVLA imekuwa ikifanya kazi muhimu katika kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya mifugo, uzalishaji, usambazaji na usimamizi wa matumizi bora ya chanjo za Mifugo pamoja na kufanya tafiti za kisayansi zinazosaidia kukuza Sekta ya Mifugo nchini. TVLA ni kichocheo muhimu katika kuhakikisha mifugo inakuwa na afya bora na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji na kipato kwa wafugaji wetu. "alisema Prof. Muhairwa.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Katikati, waliokaa) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) baada ya kuzindua bodi hiyo katika makao makuu ya wakala jijini Dar es Salaam Machi 21, 2025.



# Kiwanda cha Samaki LIFA Chatakiwa kuanza Uzalishaji

**Na. Edward Kondela – WMUV, Mara**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Edwin Mhede ameutaka uongozi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi cha LIFA Products ltd, kilichopo Manispaa ya Musoma mkoani Mara kuhakikisha kiwanda hicho kinaanza uzalishaji hivi karibuni. Dkt. Mhede alibainisha hayo Machi 20, 2025 alipotembelea kiwanda hicho kujionea ujenzi na marekebisho kadhaa yanayofanywa kabla ya kuanza rasmi kwa uzalishaji wa kuchakata mazao ya uvuvi, huku akijulishwa baadhi ya nyaraka muhimu tayari zimekamilishwa na serikali.

Alisema serikali inaudai uongozi wa kiwanda hicho kwa kutoanza uzalishaji ilhali serikali imewawekea mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kuhakikisha nyaraka muhimu kukamilishwa na kupatiwa miongozo kadhaa kutoka kwa wataalamu kutoka ngazi ya kata hadi taifa. "Lazima tufanye kazi kiwanda hiki kianze kuzalisha na kianze kusafirisha bidhaa huko duniani, tunataka tuone kitu kinafanyika hapa na kama kuna eneo lingine lolote ambalo linamkwamo serikali ya mkoa ipo, sisi tupo na wataalamu wangu wilayani, mkoani hadi taifa tupo." alisema Dkt. Mhede Aidha, aliwataka wataalamu kutoka wizarani kufika katika kiwanda hicho mara kwa mara ili kuusaidia uongozi wa kiwanda kuhakikisha wanatoa bidhaa bora mara watakapoanza uzalishaji.

> *"Lazima tufanye kazi kiwanda hiki kianze kuzalisha na kianze kusafirisha bidhaa huko duniani, tunataka tuone kitu kinafanyika hapa na kama kuna eneo lingine lolote ambalo linamkwamo serikali ya mkoa ipo, sisi tupo na wataalamu wangu wilayani, mkoani hadi taifa tupo."*
>
> **Dkt. Edwin Mhede**
> Naibu Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)

Naye Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mara, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma Bw. Juma Chikoka alisema anataka kuona uzalishaji kwa kuwa serikali imeendelea kurahisisha na kuwajengea mazingira mazuri wawekezaji. "Kiongozi hapa amefika, amerudi tena, maana yake dhamira yake na serikali ni njema, tusiangushe tena hili jambo, maana yake hili jambo likianguka Musoma na serikali ya wilaya tupo, mimi siyo muumini wa kuanguka." alisema Bw. Chikoka. Pia, aliahidi kurudi katika kiwanda hicho Mwezi Aprili mwaka huu ili kujionea maendeleo ya kiwanda na kupata taarifa rasmi ya kuanza kwa uzalishaji wa kuchakata mazao ya uvuvi, hivyo kukamilisha mapema masuala ya kitaalamu. Kwa upande wake Meneja wa Kiwanda cha LIFA Products ltd. Bw. Mwita Masumbo alikiri kuwa kiwanda hicho kinadaiwa na serikali kwa kutoanza uzalishaji licha ya kukabidhiwa nyaraka muhimu zinazowaruhusu kuanza kuchakata mazao ya uvuvi. Alisema uongozi wa kiwanda utafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kiwanda kinaanza uzalishaji hivi karibuni.



# WANAFUNZI FETA WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA YA MIKOPO

*Ni wale wanaotarajia Kujiunga na Masomo 2025/2026*

**Na Maria Mtambalike - FETA, Pwani**

Wanafunzi wanaotarajia kujiunga na Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), watakiwa kuchangamkia fursa ya mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Masomo 2025/2026.

Rai hiyo ilitolewa Machi 26, 2025 na Afisa Udahili FETA Bw. Musa Mndeme wakati akitoa taarifa ya uwepo wa fursa ya mikopo ya elimu inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi wanaojiunga na kozi mbalimbali zinazotolewa na FETA.

Bw. Mndeme alisema kuwa kwa Mwaka wa Masomo 2024/2025 wanafunzi 19 wamenufaika na mkopo huo kwa kulipiwa gharama za ada,malazi nachakula ambapo inadaiwa kuwa idadi ya wanufaika wa mikopo imekuwa ndogo kwa sababu wanafunzi wengi walikuwa hawana taarifa na uelewa juu ya uwepo wa fursa ya mikopo hiyo.

Akielezea umuhimu wa mikopo hiyo Bw. Mndeme alisema mikopo hiyo ambayo inajumuisha gharama za ada, shajara (stationeries), chakula pamoja na malazi, italeta unafuu kwa wazazi/walezi ambao wana changamoto za kifedha kuweza kumudu gharama za elimu ya juu, hivyo watoto wao wataweza kufikia malengo yao bila kuwa na hofu ya kikwazo cha fedha.

Aidha,alibainisha kuwa uwepo wa mikopo hiyo itasaidia kuongeza wanafunzi ambao wamekua wakitamani kujiunga katika kozi zinazotolewa na FETA na kupata ajira ama kujiajiri katika Sekta ya Uvuvi inayokua kwa kasi.

Bw. Mndeme alitoa wito kwa wanafunzi wote wa FETA wanaoendelea na masomo na wanaotarajia kujiunga na chuo kwa mwaka 2025/2026 kuchangamkia fursa hiyo adhimu ili iweze kuwarahisishia katika ulipaji wa gharama mbalimbali wakiwa chuoni kwani wanafunzi wote watakaodahiliwa FETA wanakidhi vigezo vya kunufaika na mikopo.

> *Mikopo hii inajumuisha gharama za ada,shajara (stationeries), chakula pamoja na malazi, italeta unafuu kwa wazazi/walezi ambao wana changamoto za kifedha kuweza kumudu gharama za elimu ya juu.*
>
> Bw. Musa **Mndeme**
> Afisa Udahili - FETA



## WANAFUNZI SUA KUJIFUNZA KWA VITENDO TAFIRI, KITUO CHA DAR ES SALAAM

**Na.Herry Kilele – TAFIRI, Dar es Salaam**

Machi 26, 2025, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Kituo cha Dar es Salaam kilipokea wanafunzi saba wa mwaka wa tatu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine Kilimo (SUA) kilichopo mjini Morogoro, wanaosomea Shahada ya Sayansi ya Ufugaji wa Viumbe Maji (Aquaculture) kwa ajili ya mafunzo ya vitendo.

Wanafunzi hao waliongozwa na Afisa Uvuvi Mwandamizi kutoka TAFIRI, Kituo cha Dar es salaam Bw. Patroba Matiku ambapo katika siku ya kwanza ya mafunzo kwa vitendo, wanafunzi hao walitembelea Soko la Kimataifa la Samaki la Ferry Jijini Dar es Salaam, ambapo walikutana na Afisa Uvuvi wa Soko hilo, Bw. Abeid Shamte. Wanafunzi walipata fursa ya kujifunza kuhusu kanda mbalimbali za soko na shughuli zinazofanyika katika kila kanda ambapo walitembelea kanda nane na waliona jinsi samaki wanavyohifadhiwa katika majokofu maalumu, pamoja na shughuli za wa chuuzi katika soko hilo.

Huu ni mwendelezo wa shughuli zinazofanywa na TAFIRI Katika kuhakikisha zinawaandaa wanafunzi ambao kwa siku zijazo watatumika katika shughuli mbalimbali za utafiti katika Sekta ya Uvuvi.

# Washiriki Mafunzo ya Ufugaji Samaki kwenye Vizimba waagizwa Kuongeza Uzalishaji

**Na Maria Mtambalike – FETA, Mwanza**

Washiriki 172 wa mafunzo ya muda mfupi ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba wametakiwa kutumia vyema mafunzo hayo ili kuongeza uzalishaji wa samaki nchini.

Wito huo ulitolewa Machi 28, 2025 na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtandawakati akifunga mafunzo na kutunuku vyeti kwa washiriki 172 waliomaliza mafunzo ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba yaliyofanyika FETA –Kampasi ya Nyegezi.

Mhe. Mtanda alibainisha kuwa takwimu za hivi karibuni zinaonesha kumekuwa na upungufu mkubwa wa uzalishaji samaki na kutokana na uvuvi haramu, mabadiliko ya tabia ya nchi, uharibifu wa mazingira pamoja na ongezeko la wavuvi ukilinganisha na ongezeko la rasilimali za uvuvi zilizopo, hivyo kupitia mafunzo hayo ana imani washiriki watafanya mageuzi chanya katika kuongeza uzalishaji wa samaki kwa njia bora zaidi.

Kwa upande wake Meneja wa FETA Kampasi ya Nyegezi Bw. Stephen Lukanga alisema, FETA kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inawashukuru wafadhili EU-EAC na TRUEFISH kwa kuwezesha mafunzo hayo ambayo yatawezesha vijana kujiajiri na kuajiri watu wengine juu ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba. Aidha,alisema FETA inaahidi kuendelea kushirikiana na washiriki waliomaliza mafunzo yao ili kuhakikisha miradi watakayokwenda kuanzisha inakuwa na weledi na kuleta tija kwa taifa.

Naye, mratibu wa mafunzo hayo Bw. Jimy Masumbuko alisema kwa siku 15, washiriki walipata ujuzi juu ya ukuzaji wa samaki kibiashara, masoko ya samaki, uhakiki ubora wa maji, afya na magonjwa ya samaki, mifumo ya ukuzaji samaki, uundaji, usimikaji na uhudumiaji wa samaki kwenye vizimba pamoja na utengenezaji wa chakula cha samaki na ulishaji wa samaki kwenye vizimba.

Mengine ni uzalishaji wa mbegu bora za samaki, uogeleaji na uendeshaji wa vyombo vya uvuvi, uthibiti wa upotevu wa samaki baada ya mavuno na uongezaji wa thamani wa mazao ya samaki. Mafunzo hayo ya siku 15 yalianza Machi 10, 2025 na kuhitimishwa Machi 28, 2025 yakihusisha wafugaji samaki, maafisa uvuvi na wajasiriamali.



# MATUKIO KATIKA PICHA

**Kikao cha Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji na Menejimenti na Watumishi wa Wizara kilichofanyika Machi 25 na 26 mwaka 2025 katika ofisi za Wizara zilizopo Mtumba Jijini Dodoma.**











# MATUKIO KATIKA PICHA

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alipofanya mazungumzo kuhusu ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia katika sekta za mifugo na uvuvi mara baada ya kutembelewa na baadhi ya maafisa kutoka benki hiyo wakiongozwa na Meneja wa Masuala ya Kilimo Kusini na Mashariki mwa Afrika Bi. Frauke Jungbluth pamoja na baadhi ya watumishi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mazungumzo hayo yalifanyika katika ofisi ndogo za wizara zilizopo jengo la NBC jijini Dodoma, Machi 11, 2025.









# MATUKIO KWENYE PICHA

Shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Viongozi na Wataalamu wa Wizara ya mifugo na uvuvi katika kipindi cha mwezi machi mwaka 2025 katika maeneo mbalimbali nchini.


















# MATUKIO KWENYE PICHA

Ziara ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti alipotembelea na kukagua mashamba ya serikali ya kuzalishia mifugo yaliyochini ya Ranchi za Taifa NARCO kuanzia Mei 06 hadi 10 mwaka 2025 kwa kuifikia mikoa ya Mbeya, Rukwa na kagera .











# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

Wizara ya Mifugo na Uvuvi